



Hapo zamani katika ikulu
kubwa, paliishi mfalme na
bintiye mrembo.




Wakati huo,
kukashuhudiwa kiangazi
kikubwa katika nchi ile.
Mfalme alikuwa na wazo
kisho akawaita majirani
zake kwenda ikuluni.




Mfalme aliwaambia Ndovu na Kinyonga, "Ninataka mkanyage ardhi hadi maji yapatikane." Mfalme aliahidi kuwa ambaye angefaulu angemwoa bintiye wa kifalme.



Kinyonga hakuwa na matumaini yoyote kwa ajili ya udogo wake. Ndovu alifurahi mno kwani alikuwa na umbo kubwa na mwenye nguvu. Ndovu alienda uwanjani na kuanza kukanyaga aridhi.



Vumbi nyingi ilitokea,
lakini hapakuwa na maji.
Ndovu alikanyaga aridhi
mpaka karibu maji
yatokee, lakini alielekea
kuchoka. Alimwachia
Kinyonga nafasi kujaribu.



Kinyonga alianza
kukanyaga aridhi. Baada
ya muda mfupi, maji
yalitoka. Watu
hawakuamini macho yao!



Kwa hivyo, Mfalme alimpa
Kinyonga bintiye. Ndovu
alienda nyumbani kwa
hasira.



Kwa hivyo, Mfalme alimpa
Kinyonga bintiye. Ndovu
alienda nyumbani kwa
hasira.